Arrivals" yaani wageni wanaotoka nje ya nchi.

Jengo hilo lilikuwa na migahawa na ofisi mbalim-

mmoja ofisa uhamiaji, alikuwa mwanamke mrefu na mweupe mwenye haiba ya

simu.

"Kwani ukoje na Lilanie?" Ofisa mmoja wa uhamiaji

Udaktari wa Falsafa katika Sheria aliyoipata akiwa na

na kunizindua toka kwenye mawazo yaliyoanza kuniteka.

ITAENDELEA

» MAPENDEKEZO TUME YA HAKI JINAI

# Kipaumbele, utawala bora na haki za binadamu

Na Monica Mnanka

KATIKA juhudi za kuimarisha ulinzi wa haki za binadamu, uzingatiwaji wa misingi ya utawala bora na kurejesha imani ya wananchi katika mfumo wa haki jinai, Januari 31, 2023, Rais Samia Suluhu Hassan alizindua Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai iliyoongozwa na Jaji Mkuu mstaafu Mohamed Chande Othman.

*Tume ilifanya kazi kwa takribani miezi sita kisha ilikabidhi ripoti yake kwa Rais, Julai 15, 2023.*

*Lengo la kuundwa kwa tume hiyo lilikuwa kupata ushauri wa namna ya kuboresha utendaji kazi wa taasisi zinazohusika na haki jinai nchini, hivyo kushughulikia malalamiko ya wananchi yanayohusu mfumo wa haki jinai.*

Rais Samia alifikia hatua hiyo kutokana na malalamiko ya muda mrefu ya wananchi dhidi ya taasisi za haki jinai kuhusu ukamataji watu pasipo kuzingatia sheria, na ubambikizwaji wa kesi.

Mengine yalikuwa ucheleweshaji wa kesi, msongamano wa wafungwa na mahabusu gerezani, masharti magumu ya dhamana na matumizi mabaya ya madaraka.

*Malalamiko kama hayo yanagusa moja kwa moja misingi ya utu, ubinadamu na ustawi wa jamii inayojengwa juu ya haki na utawala bora.*

*Mapendekezo yaliyotolewa na tume kuhusu namna ya kuboresha utendaji wa taasisi za haki jinai yalitokana na matokeo ya utafiti na ushauri uliohusisha wadau mbalimbali wakiwemo viongozi wa serikali, taasisi za umma, vyama vya siasa, viongozi wa dini, waathirika wa mfumo* wa haki jinai, asasi za kiraia na wananchi. Aidha, uzoefu wa nchi nyingine pia ulizingatiwa.

Taasisi zilizotajwa kwenye mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai ni Mahakama ya Tanzania, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA).

Taasisi nyingine ni pamoja na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Idara ya Uhamiaji, Wakala wa Huduma za Misitu (TFS), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA), Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (Tanapa), Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Idara ya Ustawi wa Jamii, Idara ya Huduma kwa Jamii, Bodi ya Parole na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA).

Haki za binadamu nchini Tanzania zinalindwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Mwaka 1977 na kuainishwa katika sheria mbalimbali za nchi pamoja na mikataba ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imeridhia.

Ulinzi wa haki hizo hauishii katika maandishi ya sheria pekee, bali pia uzingatiwaji wake unaakisiwa katika matendo ya viongozi, watendaji wa taasisi zilizomo katika mnyororo wa mfumo wa haki jinai na wananchi.

Kwa upande wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) ikiwa ni taasisi ya kitaifa ya haki za binadamu ambayo kikatiba inalo jukumu la kukuza na kulinda haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini pamoja na majukumu iliyonayo kikatiba na kisheria iliongezewa jukumu lingine kutokana na mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai la kushughulikia malalamiko ya wananchi yanayotokana na utendaji wa taasisi za haki jinai.

Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa na Serikali katika utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai katika tume hiyo ni kuanzishwa kwa Kitengo cha Taasisi za Haki Jinai Mwaka 2025 chenye wajibu wa kushughulikia malalamiko dhidi ya taasisi za haki jinai yanayohusu uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora.

Kupitia muundo huo mpya wa tume ya utawala bora ulioidhinishwa na Rais Samia, Machi 29, 2025 yameainishwa majukumu yanayopaswa kutekelezwa na kitengo husika ili kuimarisha upatikanaji wa haki katika taasisi za haki jinai.

Majukumu hayo ni pamoja na kupokea malalamiko ya wananchi yanayohusisha uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora toka katika taasisi za haki jinai.

Majukumu mengine ni kufanya uchunguzi wa malalamiko au taarifa zinazohusiana na uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora kutoka taasisi za haki jinai na kuwezesha usuluhishi.

Mengine ni upatanishi na maridhiano baina ya wananchi na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za kila siku za taasisi za haki jinai ili kubaini iwapo zinafanyika kwa kuzingatia misingi ya haki za binadamu na utawala bora.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai nchini, uundwaji wa Kitengo cha Kushughulikia Malalamiko ya Wananchi dhidi ya Taasisi za Haki Jinai ni jibu kwa kiu ya muda mrefu ya wadau wa haki za binadamu ya uwepo wa chombo cha kiraia kwa ajili ya kusimamia uwajibikaji na utekelezaji wa majukumu ya taasisi zinazohusika na masuala ya haki jinai.

**Mwandishi ni Mkurugenzi, Idara ya Elimu kwa Umma, Mawasiliano, Utafiti na Nyaraka. Aidha, ni Msemaji Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**